# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

### TANGAZO LA ZABUNI YA KUKODISHA KANTINI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO ZABUNI NA. LGA/BDC/2024/2025/NC/01.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anawatangazia wananchi wote kuwa anakodisha sehemu ya kantini iliyopo katika Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo Makao Makuu. Hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anakaribisha maombi ya kukodisha Kantini kwa wazabuni wenye uzoefu katika kutoa huduma ya chakula na Viburudisho.

**SIFA ZA MUOMBAJI**

i. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
ii. Mwombaji lazima awe na namba ya utambulisho ya mlipa kodi (Tin Number)
iii. Mwombaji lazima awe na leseni hai ya Biashara.
iv. Mwombaji lazima andike barua ya maombi kwa jina la Kampuni au jina la biashara
v. Mwombaji awe amewahi kufanya kazi ya kutoa huduma ya chakula na viburudisho katika taasisi za Umma na Mashirika, ambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha kuwa amewahi kufanya kazi na serikali , nakala kama Mkataba wa kazi/LPO, Hati za malipo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2022 mpaka 2025
vi. Mwombaji lazima aambatanishe barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji Kijiji/Mtaa
vii. Mwombaji atatakiwa kulipia Gharama ya maombi ya Zabuni kiasi cha shilingi za Kitanzania elfu hamsini tu (50,000/=) kabla ya kuwasilisha barua ya maombi.
viii. Malipo yote ya maombi ya Zabuni yalipwe kwenye Account ya Halmashauri, Kabla ya kuwasilisha barua ya maombi, waombaji watafika Ofisi ya mapato iliyopo Halmashauri ili wapate namba ya kumbukumbu ya malipo (Control Number).
ix. Mwombaji lazima awe na mashine ya kutolea risiti za kielektroniki (EFD Machine).
x. Mwombaji katika barua yake ya Maombi Lazima ataje kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa Mwezi.
xi. Bahasha ifungwe kwa lakiri na Kuandikwa Namba ya Zabuni (LGA/BDC/2024/2025/NC/01)



CamScanner
CamScanner

xii. Maombi yote yawasilishwe Ofisi ya MKurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo S.L.P 2, Tukuyu. Kuanzia tarehe 03/6/2024 na Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 10/06/2025 saa 04:30 asubuhi.

**NB:*Maombi yote ambayo hayataambatanishwa na nyaraka zilizoorodheshwa katika sifa za mwombaji hayatafanyiwa kazi.***

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUSOKELO

DKT. Joseph Ligoha
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**



CamScanner
CamScanner